ACTFL
Language Proficiency & Performance
EXCLUSIVELY THROUGH LTI

# Maswali kuhusu AAPPL Nyumbani

## 1. AAPPL ni nini?

AAPPL ni kifupi cha 'ACTFL Assessment of Performance toward Proficiency in Languages®'. Ni tovuti ya mtandaoni ya majaribio ya lugha inayohusisha sehemu nne (4) kwa lugha nyingine "moduli," kwa kutegemea na kile ambacho mwalimu au shule imechagua kwa ajili ya wanafunzi. Moduli hizi nne zinapima usikilizaji, usomaji, uongeaji na uandishi katika lugha ya dunia. Mwalimu au shule atakutaarifu ni moduli gani kati ya hizi nne zimeagizwa, kulingana na kiwango cha ustadi cha anayefanya jaribio pamoja na malengo ya jaribio husika. Unaweza kupata taarifa zaidi kupitia AAPPL Central.

## 2. Je, ni vigumu kusimamia AAPPL nyumbani?

Hapana. Ni jambo rahisi! Wasimamizi wanatakiwa kuwa wazazi, walezi, au mtu mzima yeyote anayeaminika. Baadhi ya wajibu wa msimamizi ni:

- kuhakikisha kuna mazingira salama, na yasiyo na kelele kwa majaribio,
- kuhakikisha Kompyuta na vifaa vingine vinafanya kazi vizuri kabla ya kuanza jaribio na kisha kutazama mazingira kwa ujumla wakati wa jaribio,
- kuhakikisha anayefanya jaribio hatumii karatasi, kalamu, penseli, madaftari, kamusi, simu ya mkononi, kamera au vifaa vya kielektroniki wakati wa jaribio,
- kumsaidia anayefanya jaribio anapokutana na changamoto yeyote ya kiufundi, kwa kuwasiliana na shule pamoja na/au LTI ili kupata msaada.

Orodha vitu vya kuzingatia na mwongozo kwa msimamizi vinatolewa zaidi chini katika nakala hii.

## 3. Je, jaribio la AAPPL litakuwa ni tofauti kwa sababu linafanyikia nyumbani?

Hapana. Hakuna tofauti kati ya jaribio la AAPPL linalofanyikia shuleni na linalofanyikia nyumbani.

## 4. Je, jaribio la AAPPL linachukua muda gani?

Jaribio halina muda maalumu; hata hivyo, kila moduli ya AAPPL inachukua kati ya dakika 30 mpaka 40. (Moduli ya uandishi inaweza kuchukua mpaka saa moja.) Jaribio zima linakadiriwa kuchukua masaa 2.5 kwa ujumla. Wanaofanya jaribio wanaweza kuchukua mapumziko katikati ya moduli, au kuzikamilisha kwa kipindi cha siku kadhaa, au pia wanaweza kukamilisha moduli moja kwa mkao mmoja.

## 5. Je, ninahitaji kifaa chochote kufanya jaribio la AAPPL?

Ndiyo. Utahitaji kompyuta, intaneti, vifaa vya kusikiliza sauti masikioni au spika. Na nyongeza, wanaofanya jaribio watahitaji kipaza sauti '*microphone'* kwa ajili ya kurekodi majibu yao kwa ajili ya kusikilizwa na mtu wa upande wa pili. Kompyuta nyingi siku hizi tayari zina vitu hivi, jambo linalomaanisha unaweza usihitaji kifaa kingine cha ziada. Ili kuwa na uhakika, tafadhali pitia Mahitaji ya Kiufundi na kisha Jaribu Mfumo Wako kabla ya kuanza jaribio hili. Kama unahitaji mwongozo wa ziada kabla ya kuanza, tafadhali wasiliana na shule.

## 6. Je, kuna usalama ndani ya AAPPL?

Ndiyo. AAPPL ina vipengele kadhaa vya kiusalama. Kwanza, mtu anayefanya jaribio ni lazima atoe ahadi ya uaminifu mwanzo wa kila moduli ya AAPPL. Pili, watatolewa nje ya jaribio moja kwa moja kama watahama katika jaribio na kufungua programu nyungine, dirisha lingine katika 'browser', au kichupo 'tab'. Vipengele vingine ambavyo vimesitishwa moja kwa moja ni pamoja na:


Last edited
3/10/2023 6:06 PM

- uwezo wa kubonyeza kitufe cha kulia katika ‘mouse’,
- kitufe cha kurudi nyuma katika ‘browser’,
- njia za mkato katika kibodi za Kunakili, Kubandika, na Kukata (Ctrl + c, Ctrl + v, and Ctrl + x),
- kiendelezi cha Kutafsiri cha Google katika browser, kama kimewekwa.

Wakati wa jaribio, watu wanaofanya jaribio hawatakiwi kuwa karibu na vitu vilivyokatazwa, ikiwemo karatasi, kalamu, penseli, madaftari, kamusi, simu ya mkononi, kamera, na vifaa vingine vya kielektroniki.

## 7. Je, kuna rasilimali zingine zinazopatikana kwa ajili ya kufanya mazoezi kabla ya jaribio?

Ndiyo. Kama muda unakuruhusu, unatakiwa kupitia Video za Dondoo za Kufanya Jaribio za ACTFL na watu wanaofanya jaribio wanatakiwa kukamilisha jaribio la Mfano.

## 8. Je, niwasiliane na nani kama nikihitaji msaada?

Kama ukihitaji msaada wa kitaalamu, tafadhali wasiliana na shule yako kwa ushauri na mwongozo.

ACTFL
Language Proficiency & Performance
EXCLUSIVELY THROUGH LTI

# AAPPL At-Home Testing Guide

Asante kwa kusaidia katika kuwezesha ukuaji wa elimu mashuleni, kwa wanafunzi na waalimu kwa ujumla katika kipindi hiki cha mabadiliko na kuwa darasa la mbali kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19; ushiriki wako kama msimamizi wa AAPPL Nyumbani ni wa muhimu na umepokelewa kwa shukrani. Tafadhali kumbuka kwamba wasimamizi wa majaribio wanatakiwa kuwa ni wazazi, walezi au watu wazima wengine wanaoaminiwa ambao wanaweza kulinda eneo la majaribio. **Mwongozo wa Jaribio** huu utakusaidia kujiandaa kuendesha jaribio nyumbani kwa ukamilifu.

## Viunga vya Haraka

| | |
|---|---|
| **MFANO WA AAPPL:** | https://www.languagetesting.com/aappl2-demo |
| **JARIBU MFUMO WA AAPPL:** | https://aappl2.actfltesting.org/systemcheck |
| **MAHITAJI YA KIUFUNDI:** | https://www.languagetesting.com/aappl2-demo |
| **KUFANYA JARIBIO:** | https://aappl2.actfltesting.org |

## Orodha ya Vitu ambavyo Msimamizi wa Nyumbani anatakiwa Kuvifanya

- ❑ Kupitia Mahitaji ya Kiufundi, kuweka mipangilio katika kompyuta itakayotumika kwa jaribio, na Kujaribu Mfumo mzima.
- ❑ Kuhakikisha watu wanaofanya jaribio wanapitia Mifano na kujaribu kibodi zao kwa ajili ya kipengele cha Uwasilishaji wa Uandishi.
- ❑ Kupanga muda na mgawanyiko wa vipengele mpaka vinne vya majaribio utakavyovitoa (waalimu wako au shule yako itatoa muongozo wa hilo). Kila kimoja kinachukua dakika 30-45, na mpaka dakika 60 kwa kesi ya Uwasilishaji wa Uandishi.
- ❑ Andaa mazingira salama ya kufanyia majaribio na uwe na taarifa za kuingilia karibu. Kumbuka kwamba watu wanaofanya jaribio hawatakiwi kuwa na karatasi, kalamu, penseli, madaftari, kamusi, simu ya mkononi, kamera au kifaa chochote cha elektroniki wakati wa jaribio.
- ❑ Mfungulie anayefanya jaribio kwa kutumia taarifa za kuingilia ambazo zimetolewa na mwalimu au shule.
- ❑ Msimamie anaefanya jaribio ukihakikisha anakamilisha vipengele vyote na kulinda taarifa zao za kuingilia katikati ya ufanyaji mzima wa jaribio. Usimsaidie kujibu swali lolote katika AAPPL.
- ❑ Teketeza/futa taarifa zote za kuingilia za mfanya jaribio punde tu baada ya kumaliza vipengele vyote.